SERIKALI KUU

BARUA YA KULINDWA

DHIDI YA UKEKETAJI WA WANAWAKE

Unapaswa kutembea na barua hii ya ulinzi kila wakati unaposafiri nje ya nchi. Hatua hii inakuwezesha kuonyesha familia yako kwa uwazi kuwa nchini Ujerumani, ukeketaji wa wanawake ni kosa ambalo linaweza kusababisha ufungwe gerezani kwa miaka mingi.

Serikali Kuu ya Jamhuri ya Ujerumani

Federal Ministry
of Education, Family Affairs, Senior Citizens,
Women and Youth

Karin Prien
Federal Minister of Education, Family
Affairs, Senior Citizens, Women and Youth

Federal Ministry
of the Interior

Alexander Dobrindt
Federal Minister of the Interior

Federal Foreign Office



Johann Wadephul
Federal Minister for
Foreign Office

Federal Ministry
of Justice and
Consumer Protection

Dr. Stefanie Hubig
Federal Minister of Justice
and protection

Federal Ministry
of Health

Nina Warken
Federal Minister of Health

Ukeketaji wa wanawake ni kosa na ni ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu wenye madhara ya kudumu na makubwa ya kimwili na akili kwa wasichana na wanawake walioathiriwa. Utaratibu wa ukeketaji wa wanawake unaweza pia kusababisha kifo moja kwa moja kutokana na kuvuja damu nyingi au kupata maambukizi hatari.

Nchini Ujerumani, kutekeleza kitendo cha ukeketaji wa wanawake ni kosa la uhalifu ambalo adhabu yake ni kufungwa gerezani kwa kipindi cha hadi miaka 15.

Ukeketaji wa wanawake ni uondoaji wa sehemu fulani au sehemu yote ya nje ya siri ya mwanamke; katika njia ambayo ni hatari zaidi, tundu la uuke hushonwa na kufungwa karibu lote.

Ninapaswa kufanya nini na barua hii?

Unaweza kutembea na barua hii ya ulinzi na kuonyesha familia yako katika nchi yako ya asili. Barua hii inafafanua kuwa utekelezaji wa kitendo cha ukeketaji wa wanawake ni **kosa la uhalifu** nchini Ujerumani – hata kama kinatekelezwa nje ya nchi. Inafafanua kuwa unakabiliwa na adhabu ya **kifungo cha hadi miaka 15 gerezani** ukitekeleza kitendo cha ukeketaji wa wanawake kwa mtoto wako wa kike au ikiwa mtu mwingine atatekeleza kitendo cha ukeketaji wa wanawake na huzuii kitendo hicho au hata kushikiri katika kitendo hicho. Unaweza pia kukatazwa kuingia Ujerumani au kunyang’anywa kibali cha kuishi nchini.

Kosa la uhalifu (kifungu cha 226a cha Sheria za Uhalifu)

Chini ya sheria ya Ujerumani, kutekeleza kitendo cha ukeketaji wa wanawake ni kosa la uhalifu (kifungu cha 226a cha Sheria za Uhalifu). Mtu yeyote anayetekeleza kitendo cha ukeketaji wa wanawake anatekeleza kosa la uhalifiu na anakabiliwa na adhabu ya kifungo cha hadi miaka 15.

Kitendo cha ukeketaji wa wanawake pia kinaadhibiwa ikiwa kitatekelezwa **nje ya nchi** au ikiwa mtu anayekitekeleza ni Mjerumani au ikiwa msichana au mwanamke anayekeketwa ni Mjerumani au anaishi au makao yake makuu ni Ujerumani.

Mtu yeyote anayemsaidia mtu mwingine nchini Ujerumani au nje ya nchi katika kutekeleza kitendo cha ukeketaji wa wanawake pia anatekeleza kosa la uhalifu.

Mtu yeyote anayeshawishi wengine kutekeleza kitendo cha ukeketaji wa wanawake pia anatekeleza kosa la uhalifu.

Hii inajumuisha wazazi ambao hawalindi watoto wao wa kike dhidi ya kukeketwa nchini Ujerumani au nje yanchi.

Msichana au mwanamke aliyekeketwa halaumiwi na hataadhibiwa.

Watu wanaotekeleza kitendo cha ukeketaji wa wanawake, wanaoshawishi wengine kuwasaidia kutekeleza kitendo hicho au wanaoshindwa kulinda watoto wao wa kike dhidi ya kukeketwa wanaweza pia kunyang’anywa kibali cha kuishi nchini na wanaweza kukatazwa kuingia nchini Ujerumani.

Ukeketaji wa wanawake ni nini?

Ukeketaji wa wanawake ni **ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu** ambapo sehemu fulani au sehemu yote ya siri ya nje na/au sehemu ya ndani ya kuta za uuke na kinembe huondolewa na (katika tukio baya zaidi) uuke hushonwa na kufungwa na wakati mwingine kuacha tu tundu dogo zaidi. Wasichana wanaweza kuvuja damu nyingi sana wakati wa kutekelezwa kwa kitendo hicho au kidonda kinaweza kupata maambukizi, hali ambayo inaweza kusababisha **madhara hatari ya afya** na hata **kifo**.

- **Uchungu wa kudumu, hofu akilini**
- **Matatizo ya kujifungua, maambukizi sugu**
- **matatizo ya kupata hisia na kuhisi uchungu wakati wa kufanya ngono**

Wanawake ambao wamekeketwa hawateseki tu kutokana na **uchungu wa kudumu, hofu akilini na matatizo ya kujifungua.** Wanaweza pia kupata maambukizi sugu ya figo au kibofu na mara nyingi huumia kutokana na uchungu wa hedhi.

Majeraha ya kimwili na akili hukiuka pia vibaya sana haki za wanawake na wasichana za kujitambua kijinsia. Mara nyingi huhisi uchungu mwingi zaidi wakati wa kufanya ngono; hisia za ngono hupungua kwa kiwango kikubwa au kukosekana kwa sababu ya kuharibiwa kwa tishu ya neva.

Baada ya kutekelezwa, kwa kawaida hali ya kukeketwa **huwa ya kudumu**.

Ninaweza kupata usaidizi wapi? Ninapaswa kufanya nini ikiwa ninashuku kuwa nitakeketwa?

Ikiwa una wasiwasi kuwa wewe au mtu unayemfahamu yuko katika hatari ya kupelekwa katika nchi nyingine ili kukeketwa au ikiwa kuna hatari kama hiyo nchini Ujerumani, unaweza kuwasiliana na

- **polisi (nambari ya simu: 110) au**
- **ofisi ya masuala ya vijana ya eneo lako**.

Huduma ya kitaifa ya usaidizi kwa Dhuluma dhidi ya Wanawake hutoa msaada kupitia simu au gumzo la mtandaoni.

HILFE TELEFON
GEWALT GEGEN FRAUEN
08000 116 016

- Nambari ya simu: 08000 116 016
- www.hilfetelefon.de

Huduma ya usaidizi hutoa ushauri katika lugha 18 – wakati wowote, bila malipo na bila kukutambulisha.

Ikiwa uko nje ya nchi na unahitaji usaidizi, unaweza kuwasiliana na idara ya ubalozi wa Ujerumani.

Kijerumani:
www.auswaertiges-amt.de/de/ReiseUndSicherheit/deutsche-auslandsvertretungen

Kiingereza:
www.auswaertiges-amt.de/en/aussenpolitik/laenderinformationen

BARUA YA KULINDWA DHIDI YA UKEKETAJI WA WANAWAKE
JAMHURI YA UJERUMANI 2025

Chapa

Barua hii ya ulinzi ni sehemu ya kazi ya mahusiano ya umma ya Serikali Kuu; inapatikana bila malipo na haikusudiwi kuuzwa.

Imechapishwa kwa niaba ya Serikali Kuu na:
Bundesministerium für Bildung,
Familie, Senioren, Frauen und Jugend
Referat Öffentlichkeitsarbeit
11018 Berlin
www.bmbfsfj.bund.de

Ikiwa una maswali yoyote, piga simu kwa
nambari yetu ya huduma: +49 30 20 179 130
Jumatatu–Alhamisi: Saa tatu asubuhi hadi
saa kumi na mbili jioni (9 am – 6 pm)
Faksi: +49 30 18 555-4400
Barua pepe: info@bmbfsfjservice.bund.de

Nambari ya simu ya huduma kwa umma ya mashirika yote ya serikali na ofisi: 115*

Imechapishwa mnamo: Desemba 2025, Toleo la 5 (swahili)
Muundo: www.zweiband.de
Mchapishaji: MKL Druck GmbH & Co. KG

* Kwa maswali ya jumla kwa mashirika na ofisi zote za serikali, nambari ya huduma kwa umma ya 115 inapatikana pia. Katika maeneo yanayoshiriki, nambari ya 115 inapatikana kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kati ya Jumatatu na Ijumaa. Simu zinazopigwa kwa 115 kutoka kwa simu ya umma ya Ujerumani na mitandao mingi ya simu za mkononi hutozwa kulingana na ada ya eneo uliko na kwa hivyo hazilipishwi kwa wanaotoza ada zisizobadilika. Viziwi wanaweza kupata maelezo kwa kupiga simu kwa anwani ya SIP 115@gebaerdentelefon.d115.de. Ili ufahamu iwapo huduma ya 115 inapatikana katika eneo lako na kwa maelezo zaidi kuhusu nambari ya huduma kwa umma, tafadhali tembelea http://www.d115.de.